**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**CHUO CHA UALIMU NACHINGWEA**

Simu : 0732933334
Fax : 0732933334
E mail: **nachingweatc@gmail.com**
au **nachingweatc@moe.go.tz**
***Website: www.nachingweatc.ac.tz***

S. L. P. 39,
**Nachingwea**.
31.05.2023

Unapojibu tafadhali nakili:
**Kumb: Na. NCCU/A.3/6/34**
**N**dugu, ……………………………………..

……………………………………..

**YAH: KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA STASHAHADA YA UALIMU WA ELIMU YA SEKONDARI (SAYANSI JAMII NA LUGHA) AU ASTASHAHADA YA UALIMU ELIMU YA AWALI/MSINGI KWA MWAKA WA MASOMO 2023/2024**

**UTANGULIZI:**

**N**inapenda kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga na mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Sekondari (Sayansi jamii na lugha) / Astashahada ya Elimu ya Ualimu Elimu ya Awali/Msingi katika Chuo cha Ualimu Nachingwea.

Mwelekeo wa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia ni kumwandaa mwalimu mahiri na mwenye ujuzi stahiki katika Elimu ya Ualimu. Aidha mafunzo utakayopata yatakupatia sifa na ujuzi wa kufundisha hapa nchini na nje ya nchi kwa kuzingatia fursa za soko la ajira ndani na nje ya nchi. Elimu ya Ualimu ni msingi mkuu katika utoaji wa Elimu na imepewa kipaumbele katika sera mpya ya Elimu na mafunzo ya mwaka 2014.

Uongozi na jumuiya yote ya Chuo cha Ualimu Nachingwea wanakupongeza kwa kuchaguliwa kujiunga na mafunzo ya Ualimu katika Kozi ya **Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Sekondari (sayansi jamii na lugha)/Astashahada ya Ualimu Elimu ya Awali/Msingi** katika chuo hiki. Ufikapo lango la chuo utakutana na kauli mbiu ya chuo "**Nitajielimisha**" na maneno:-"Ni **Tunu kuwepo katika Chuo hiki, kitunze kiwe safi mara zote**". Itumie vizuri Tunu hiyo ili kupata maarifa na stadi bora ili kujenga mwelekeo unaokubalika katika Taaluma ya Ualimu.

**MAHALI CHUO KILIPO.**

Chuo hiki kipo katika Mkoa wa Lindi, Wilaya ya Nachingwea, umbali wa kilometa moja kutoka stendi kuu ya mabasi Nachingwea mjini. Kuna usafiri wa mabasi kila siku kwenda Nachingwea kupitia Masasi kutoka Dar es salaam. Unashauriwa kutumia usafiri wa kampuni ya mabasi ya **NAVIL, MANING NICE** na **MACHINGA** ambao usafiri wake upo kila siku.

**MAFUNZO**:

Chuo kitafunguliwa tarehe 17**/07/2023** na usichelewe zaidi ya tarehe **31/07/2023,** vinginevyo, hutapokelewa. Mafunzo haya ni ya muda wa miaka miwili na yanajumuisha mafunzo ya

nadharia chuoni na vitendo katika mazingira halisi ya **shule za sekondari/msingi** ambapo utatakiwa kufanya mazoezi ya kufundisha kulingana na utaratibu wa Chuo na maelekezo ya Wizara yatakavyokuwa.

Mafunzo ya Stashahada ya Ualimu wa Elimu ya Sekondari(Sayansi Jamii na Lugha)/Astashahada ya Ualimu Elimu ya Awali/Msingi yanamwandaa mwalimu wa ngazi ya Stashahada/Astashahada ya Ualimu atakayemudu kufundisha masomo yote yanayofundishwa katika Elimu ya Sekondari/Awali/Msingi.

**Vyeti na masharti ya usajili:**

**Uje na vyeti halisi na halali kama ifuatavyo**:-

1. Cheti cha taaluma (**Academic certificate**) au Hati ya matokeo **(Result slip)** kwa wale waliomaliza mwaka 2022 kwa kidato cha nne na mwaka 2023 kwa kidato cha sita ambao vyeti vyao havijatolewa na Baraza la mitihani la Tanzania.
2. Vyeti vya kuhitimu **(Leaving certificates**) kidato cha nne kwa wanachuo wa Kozi ya Astashahada, na kidato cha nne na cha sita kwa wanachuo wa Kozi ya Stashahada.
3. Cheti cha kuzaliwa **(birth certificate**)
4. Hati yoyote ya ziada inayoweza kusaidia kukutambulisha na kukuthibitisha uhalali wako na uhalali wa umiliki wa nyaraka zako za kitaaluma.
5. Chuo kwa kushirikiana na vyombo vingine vya dola kina uwezo wa kubaini wale wote wanaotumia vyeti visivyo vyao au ambavyo siyo halali na watakaobainika watafikishwa mbele ya vyombo vya sheria kwa mujibu wa sheria na taratibu za nchi.

**Mahitaji ya fedha na vifaa unavyotakiwa kuleta ni kama ifuatavyo:-**

**(a) Ada/Karo ya Chuo**

- Ada ya mafunzo kwa mwaka ni Shilingi **450,000/=** Ada hii inaweza kulipwa yote au kwa awamu mbili (Shilingi **225,000/=)** katika mwaka wa mafunzo. Ada italipwa baada ya kufika chuoni kwa mfumo wa ulipaji wa maduhuli ya serikali kwa njia ya Kielektroniki (GePG) baada ya kuandaliwa namba ya malipo (control number) kwa kila mwanachuo katika ofisi ya uhasibu chuoni. Hairuhusiwi kulipa fedha taslimu kwa mhasibu. Utaelekezwa namna na utaratibu wa kulipa ada utakapofika chuoni. Namba ya mhasibu ni **0785551600** kwa mawasiliano zaidi.

**(b) Michango**


- Serikali ya Wanachuo Tshs. 5,000/= kwa mwaka
- Afya,Usafi na Mazingira Tshs 35,000/= kwa mwaka
- Usajili na Kitambulisho Tshs. 20,000/= kwa mwaka (Kwa Mwaka wa Kwanza tu).
- Michezo Tshs. 30,000/= kwa mwaka.
- Ulinzi Tshs. 30,000/= kwa mwaka
- Vibarua Tsh 20,000/= kwa mwaka
- Ukarabati Tshs. 25,000/= kwa mwaka.
- Rim 1 ya karatasi A4 kwa mwaka
- T -shirt tsh 15,000/=
- Mahafali tsh 15,000/= kwa mwaka.
- Uje na godoro ft $2^1/_2$ kwa 6 ft**.**
- **BIMA ya afya 50400/= kwa mwaka**
- **Ada ya mitihani ya Taifa (NECTA) 50,000/= (mara moja kwa miaka miwili)**
- **Jembe likiwa na mpini wake.**

Michango hiyo yote ya kawaida **isipokuwa ada,** iingizwe kwenye akaunti ya **NACHINGWEA TTC COLLEGE FUND** akaunti namba**70403500039 iliyopo Benki ya NMB.** Unaweza ukaweka fedha hizo kwenye tawi la **NMB Nachingwea** au tawi lolote la NMB nchini na ***si vinginevyo***. **Hakikisha unakuja na risiti ulizowekea fedha hizo** (**pay in slips**) ambayo utamwonesha msajili na baadae utaiwasilisha kwa mhasibu na kukatiwa risiti ya malipo .Tunza vizuri stakabadhi utakazopewa na mhasibu chuoni ili uzitumie kuthibitisha kukamilisha michango uliyotoa itakapohitajika. **Kamilisha mahitaji hayo bila kukosa. Hautapokelewa na kusajiliwa endapo hutakamilisha mahitaji hayo.**

## MAVAZI

**Sare ya Wavulana:** Suruali ya kushona iwe ya rangi ya **“Dark Blue”** yenye mifuko pembeni mfuko mmoja wa nyuma , na rinda mbili kila upande (isiyobana). Shati bluu bahari (light blue) la mikono mirefu na lisilobana na

tai ya dark blue. Viatu vyeusi vya ngozi na soksi nyeusi. Uje na nguo za michezo (bukta, T- shirt, **Track suit** za rangi ya **Bluu** na raba za rangi yoyote isiyo nyeupe). Vilevile sweta la rangi ya blue nyeusi (Dark Blue) pamoja na koti la rangi ya 'Dark Blue' litakalofanana na rangi ya Suruali. (sweta na koti si lazima unayohiari ya kuvaa). Muonekano wa suruali unatakiwa kama ifuatavyo:



**Sare ya Wasichana:** Skirt yenye mshono wa rinda boksi ya rangi ya "**Dark Blue**" inayovuka magoti kwenda chini , shati bluu bahari **( light blue**) la mikono mirefu (lisilobana) na tai ya rangi ya "**dark blue**", viatu vyeusi vya ngozi vya kufunika vyenye visigino vifupi na soksi nyeusi . Uje na nguo za michezo (T- shirt au track suit za rangi ya **Bluu** na raba za rangi yoyote isiyo nyeupe) na sweta la rangi ya Bluu nyeusi **(Dark blue**). Muonekano wa sketi unatakiwa kuwa kama ifuatavyo:



**NB: W**anachuo wakike madhehebu ya Kiislamu wanaruhusiwa kuvaa sare ndefu za chuo na "hijab" ya kitambaa cha kichwani cha bluu bahari.

## DINI/SIASA:

Chuo kama taasisi ya serikali hakina dini/chama cha siasa. Hata hivyo, unaruhusiwa kuabudu kwa imani yako na kushiriki katika masuala ya kisiasa bila kuathiri ratiba, taratibu na kanuni za chuo. Hakikisha imani yako au ushiriki wako wa masuala ya kisiasa hauathiri taratibu za chuo wala kuvunja amani. Siasa/misimamo mikali ya dini havina nafasi hapa chuoni. Masuala ya dini/ siasa kamwe hayapaswi kuathiri taratibu za uendeshaji wa chuo.

## VIFAA VYA MALAZI, USAFI NA CHAKULA:

Unatakiwa uje na vifaa vifuatavyo kwa matumizi yako binafsi – pazia moja kwa ajili ya chumba chako lenye ukubwa wa sm 140 kwa sm 90, ndoo na vyombo vya kulia chakula. Pia uje na mashuka ya kulalia ya rangi yoyote, chandarua na mto. Vifaa hivi vilivyotajwa vinapatikana pia hapa Nachingwea mjini kwenye maduka, hivyo waweza kuamua kuja na fedha na kuvinunua huku ili kupunguza usumbufu na gharama za kuvisafirisha.

**TUNAKUTAKIA MAANDALIZI MEMA YA KUINGIA CHUNI**
**KARIBU CHUO CHA UALIMU NACHINGWEA**

**…………………………………..**
**HAMISI, M. N**
**MKUU WA CHUO**

**GOVERNMENT OF TANZANIA**

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

**PART A:**

To: Medical Officer
……………………………………….
………………………………………….
………………………………………….

From: Principal,
Nachingwea Teachers' College
P.O.Box 39,
NACHINGWEA.

Mr./Mrs./miss ………………………………………………………………… (Name in full)

Please examine the above as to is /her physical and mental fitness for a fulltime teacher training course. The examination should include the following categories (I – ii) each category or subcategory of which will render the applicant ineligible in case a defend. Pregnancy (category IV) will also render a girl candidate in eligible for the course.

1. (a) Eye – sight
   (b) Hearing
   (c) Limbs
   (e) venereal disease
   (d) leprosy
   (g) epilepsy

.................................................

Principal

……………………………………………………………………………………………………

**PART B:**

(To be completed by a government medical officer)

I have examined the above named and consider that he/ she is physical fit/ unfit and mentally fit/ unfit for a fulltime teacher course.

I. (a) Eye – sight ………………………………………………………..
   (b) Hearing ……………………………………………………………
   (c) Limbs …………………………………………………………
   (d) Speech …………………………………………………………
   (e) Venereal disease ……………………………………………………….
   (d) Leprosy ………………………………………………………..
   ii. Neurosis ………………………………………………………………..
   iii. Other serious diseases ………………………………………………..
   iv. Pregnancy ……………………………………………………………
   v. Mental and physical fitness …………………………………………..

Date ……………………………………….. Signature ……………………………………